JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

SLP 2324

elephone:0262968010
,
Fax:0262968010
Website:www.kilolodc.go.tz
.

IKLOLO
Tanzania

19/08/2023

TANGAZO LA KAZI KWA MAFUNDI UJENZI

A: UTANGULIZI:

Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imepokea fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Shule Maalumu ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Iringa , katika kata ya Lugalo ,kijiji cha Mbigili. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo anatangaza kazi kwa mafundi wenye uwezo na sifa za kujenga majengo mbalimbali ya Shule hiyo kwa mfumo wa **Force Account.** Tangazo hili liko wazi kwa umma (***Mafundi wote, mtu binafsi au Kikundi cha Mafundi ujenzi*** wenye sifa na uzoefu kwa kazi za ujenzi wa majengo ya Serikali kama ifuatavyo:

MAJENGO YA MADARASA.

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
1	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/CR/FA/W/01**	MADARASA	MADARASA MANNE NA MAWILI YENYE VYOO
2	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/CR//FA/W/02**	MADARASA	**SITA YENYE OFISI**
3	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/LB//FA/W/03**	MAABARA	**FIZIKIA,JIOGRAFIA,KEMIA NA BAILOGIA**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
4	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/ADM/FA/W/04**	UTAWALA	**1**
5	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/BWL/W/05**	BWALO	**1**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
6	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/T,H/FA/W/06**	NYUMBA YA MWALIMU,VYUMBA VITATU	**1**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
7	**LGA/027/2022/2023/RSSG/HL/FA/W/07**	MABWENI	**2**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
8	**LGA/027/2022/2023/RSSG/HL/FA/W/08**	MABWENI	**2**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
9	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/HL/FA/W/09**	MABWENI	**2**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
10	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/HL/FA/W/10**	MABWENI	**2**

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
11	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/SB/FA/W/11**	SICK BAY,CHOO,SEPTIC NA SOAKWAY	SICK BAY,CHOO,SEPTIC NA SOAKWAY

NA	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA JENGO	IDADI YA MAJENGO
12	**LGA/027/KDC/2022/2023/RSSG/INC/FA/W/12**	KICHOMEA TAKA,CHUMBA CHA JENERETA MNARA WA TANK NA TANKI LA MAJI LA CHINI UJAZO LITA 32,000	KICHOMEA TAKA,CHUMBA CHA JENERETA MNARA WA TANK NA TANKI LA MAJI LA CHINI UJAZO LITA 32,000

B: SIFA ZA MUOMBAJI.

I. Awe na uzoefu katika kazi anayoomba.
II. Awe ameshiriki katika kazi za ujenzi wa majengo ya Serikali.
III. Awe na uzoefu wa kusoma na kutafsiri michoro na ramani za ujenzi.

IV. Awe na uwezo wa kuwasimamia na kuwaongoza mafundi wote watakaokuwa chini yake.

V. Fundi awe na uwezo wa kuandaa mpango kazi na aambatanishe kwenye maombi

VI. Awe mwaminifu na mvumilivu katika kazi.

VII. Awe na uwezo wa kifedha wa kufanya kazi na kuwalipa wasaidizi wake ndani ya siku kumi na nne pasipo kuomba usaidizi wa kifedha kutoka kwa mwajiri

VIII. Fundi mkuu Awe na cheti cha taaluma ya kazi anayoomba

C: MASHARTI YA JUMLA KWA MUOMBAJI.

a. Aambatanishe nakala ya mikataba na vyeti vya malipo na **vyeti vya kumaliza kazi visipungue vitatu** , kwa kazi za ujenzi wa majengo ya Serikali aliyowahi kujenga.
b. Anatakiwa kuambatanisha nakala ya kitambulisho cha uraia au kadi ya kupigia kura.
c. Awasilishe barua ya Afisa Mtendaji wa Kijiji ikiwa na picha yake iliyogongwa muhuri wa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa
d. Aonyeshe eneo anapoishi (Kata, Kijiji / Kitongoji) na ataje namba ya simu ya Mkononi.
e. Anapaswa kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuomba zabuni ikiwa ni pamoja na kutembelea eneo la kazi (**site visit**) katika eneo la **Mbigili, kata ya Lugalo** pia kupata michoro ya kazi husika kusoma na kuielewa kabla ya kujaza mchanganuo wa kazi inapobidi ili kutoa makadirio sahihi.
f. Aambatanishe nakala ya taarifa zake za kibenki.
g. Ajaze fomu ya mchanganuo wa ufundi (Schedule of labour) kiunadhifu.
h. Aambatanishe barua ya kuomba kazi husika, na awe na **TIN namba PIA**

I. Mwombaji aambatanishe ushahidi wa kuwa ,atakuwa na vitendea kazi kama vya kuchanganyia zege ,n.k

D: JINSI YA KUTUMA MAOMBI.

1. Mafundi wenye sifa tajwa hapo juu mnaalikwa kufika na kuorodhesha majina yenu, kusaini na kuchukua kablasha la zabuni linalopatikana katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo Jumatatu hadi Ijumaa saa 2: 00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri isipokuwa siku za jumamosi na jumapili . Hakuna ada yoyote ya kulipia.

2. Fundi awasilishe barua ya kuomba kazi ya ujenzi katika ofisi ya Mkuu wa kitengo cha Manunuzi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo katika jengo la ofisi ya Mkurugenzi mtendaji chumba namba 65 ikitaja zabuni anayoomba.
3. Bahasha zote zifungwe na kuandikwa juu namba ya zabuni au aina ya jengo ulioomba na itumwe kwa:.

   KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
   HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO
   S.L.P 2324 KILOLO.

4. Kablasha ambazo zitachelewa hazitapokelewa wala kufunguliwa.
5. Mwisho wa kuchukua na kutuma maombi ni tarehe ***04/09/2023*** Jumanne **saa 4:00 asubuhi**. Maombi yatafunguliwa katika hadhara kwenye jengo la ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya KILOLO tarehe 04.09.2023 ***,saa 4:00 asubuhi,*** unaombwa kuwepo siku ya ufunguzi.

6. Barua za maombi pamoja na viambatanisho viwasilishwe kwa mkono katika ofisi tajwa hapo juu.
7. Barua zote zitumwe kwa anwani ifuatayo:

   Mkurugenzi Mtendaji,
   HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO
   S.L.P 2324 KILOLO.

Imetolewa na:

Amelye Mfugale
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHARI YA WILAYA YA KILOLO